TANGAZO LA SERIKALI NA. 460 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA KUDHIBITI UZURURAJI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI YA MWAKA 2024.

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Kudhibiti Uzururaji wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"eneo la malisho" ni eneo ambalo limetengwa na mamlaka husika kwa ajili ya malisho ya mifugo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

"kaya" maana yake ni familia ya baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi nao, au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi; "Palio" ni eneo lolote lililoko ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai linalotumika kwa ajili ya kupitishia mifugo kwenda eneo la malisho, josho au mnadani;

"mifugo" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, nguruwe na wanyama wengine wanaofugwa na binadamu;

Mifugo kutozurura ovyo

4. Kila Mfugaji ana wajibu wa kuzuia mifugo yake kuzurura au kuzagaa ovyo barabarani, mitaani, kwenye mashamba ya watu au kwenye sehemu ambazo sio malisho ya mifugo.

Udhibiti mifugo inayozurura ovyo

5.-(1) Halmashauri itakamata mfugo au mifugo yoyote itakayoonekana inazurura ovyo katika eneo la Halmashauri.

(2) kila mwenye mifugo iliyokamatwa atatozwa faini kwa kila mfugo kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hii.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2) mfugo au mifugo yoyote itakayokamatwa itatozwa faini ya utunzaji kiasi cha Shilingi elfu kumi kwa kila siku.

(4) Endapo mfugo uliokamatwa hautachukuliwa na mmiliki ndani ya kipindi cha siku saba (7) tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo huo baada ya kupata idhini ya Mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmliki wa mfugo huo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mfugo, gharama ya Mahakama na gharama ya mnada.

(5) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (4) Halmashauri kabla ya kuuza mfugo huo kwa mnada itamjulisha mmliki na umma juu ya kusudio hilo.

(6) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo au mfugo kutokana na sababu yoyote ile, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama vifo hivyo vitakuwa vimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri

Makosa na Adhabu

6. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na endapo akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki moja na hamsini elfu tu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 5 (2))*

| Na | Aina ya mifugo | Faini kwa kila mmoja |
|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe | 50,000/= |
| 2. | Mbuzi | 20,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Kondoo | 20,000/= |
| 4. | Nguruwe | 20,000/= |
| 6. | Mbwa | 20,000/= |
| 7. | Punda | 20,000/= |
| 8. | Ngamia | 20,000/= |

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 12 mwezi Mei, mwaka .

DIONIS M. MNYINGA
*Mkugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Hai*

EDMUND RUTARAKA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Hai*

NAKUBALI,

/

L.S

Dodoma,
5 Disemba, 20243

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*